**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Anuani ya simu "ELIMU"
Simu: 026 296 35 33
Baruapepe:info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S. L. P. 10,
**40479 DODOMA.**

**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb.Na. CA.229/238/01/50**

**28 Februari 2023**

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P 63088,
**DODOMA.**

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P 1454,
**DAR ES SALAAM.**

Katibu Mtendaji,
Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA),
S.L.P 21422,
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Investors in Education (TAPIE),
S.L.P 13346,
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,

Baraza la Sunnar Tanzania (BASUTA),

S.L.P 8581,

**DAR ES SALAAM.**

Mkurugenzi,

Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),

S.L.P 13547,

**DAR ES SALAAM.**

**Yah: WARAKA WA ELIMU NA. 01 WA MWAKA 2023**
**KUHUSU UBORESHAJI WA HUDUMA YA MAGARI/MABASI YANAYOTUMIKA KUSAFIRISHA WANAFUNZI**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

2. Shughuli yoyote ya utoaji wa huduma kuhusu malezi, makuzi, ujifunzaji na ustawi wa watoto kwa ujumla inapaswa kupangwa na kutekelezwa kwa makini, weledi na nidhamu ya hali ya juu kwa kuzingatia kwamba hatma ya Taifa letu, kwa kiasi kikubwa, inategemea ubora wa huduma tunazowapa watoto wetu. Kwa sababu hiyo, kila aliyekabidhiwa dhamana ya kutoa huduma yoyote ile kwa watoto lazima atimize wajibu wake kwa makini, weledi na nidhamu ya hali ya juu ili watoto wafikie kilele cha ufanisi katika makuzi, ujifunzaji na ushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo. **Thamani ya rasilimali watoto ni kubwa kuliko thamani ya rasilimali yoyote ambayo tumejaliwa kuwa nayo katika nchi yetu**.
Pamoja na ukweli huo, imebainika kuwa baadhi ya watoa huduma kwa watoto wamekuwa na tabia zenye mwelekeo wa kuleta mmomonyoko wa maadili, kuathiri ukuaji, ujifunzaji na kuhatarisha ustawi wa watoto kwa ujumla.

3. Waraka huu unalenga kuboresha utoaji wa huduma ya usafiri wa magari/mabasi kwa wanafunzi kwenda na kurudi kutoka shuleni kufuatia matukio ya ukatili dhidi ya wanafunzi yanayofanywa na baadhi ya watoa huduma ikiwemo ubakaji na ulawiti. Aidha, baadhi ya tabia za watoa huduma zina viashiria vya kuleta mmomonyoko wa

maadili, kuathiri ukuaji, ujifunzaji na kuhatarisha ustawi wa watoto kwa ujumla. Tabia hizo ni pamoja na:

a) Kuwa na watoa huduma wa jinsi moja kwenye magari/mabasi hususan wanaume;

b) Kuweka miziki/nyimbo au picha za video zisizozingatia maadili, mila, desturi na tamaduni zetu wakati wa safari za magari/mabasi hayo yakiwa yamebeba wanafunzi;

c) Wahudumu kuwafanyia vitendo vya ukatili wanafunzi wakiwa ndani ya magari;

d) Kuwa na ratiba ya safari inayoanza alfajiri (mf. Saa 11:00) na kuwalazimu watoto wadogo kukatisha usingizi usiku wa manane na hivyo kuathiri ukuaji na ujifunzaji wao;

e) Kuwa na ratiba za safari za kutoka shule zinazowafanya baadhi ya wanafunzi kufikishwa nyumbani majira ya usiku ilhali vipindi vya masomo vimeisha mapema alasiri; na

f) Kuwa na magari/mabasi yenye vioo visivyo angavu (tinted).

4. Kwa Waraka huu, **Wamiliki wote wa shule** zenye kutoa huduma za usafiri kwa wanafunzi mnaelekezwa kutekeleza yafuatayo:

a) Kila mmiliki wa shule ajitahidi kuwa na mhudumu wa kike na wa kiume katika kila gari/basi linalosafirisha wanafunzi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa safari. Inaposhindikana, mmiliki awasilishe taarifa kupitia Wathibiti Ubora wa Shule kueleza sababu zilizomfanya ashindwe kufanya hivyo. Endapo itashindikana kabisa, mhudumu wa kike atumike kutoa huduma kwenye gari/basi husika baada ya kutoa taarifa kwa Mthibiti Ubora wa Shule. Utekelezaji wa suala hili ufanyike kabla ya kuanza muhula wa pili wa masomo kwa mwaka 2023.

b) Kuacha kuweka miziki/nyimbo na picha za video zinazokwenda kinyume na maadili, mila, desturi na tamaduni zetu na badala yake kuweka miziki/nyimbo na picha za video zinazojenga maadili na uzalendo wa wanafunzi;

c) Kukomesha vitendo vya ukatili kwa wanafunzi wakiwa kwenye magari/mabasi;

d) Kuwa na ratiba rafiki za safari ili wanafunzi, hususan watoto wadogo, wapate muda wa kutosha kupumzika kwa ajili ya ukuaji wao;

e) Kuwa na magari/mabasi yenye vioo angavu (visivyokuwa tinted) yanayotumika kusafirisha wanafunzi; na

f) Wamiliki wa shule wahakikishe kwamba watumishi wanaowaajiri kutoa huduma katika magari/mabasi yanayotumika kusafirisha wanafunzi wawe waaminifu, wenye weledi na maadili. Endapo mhudumu yeyote ataenda kinyume na maadili au kuhatarisha usalama wa wanafunzi, mmiliki wa shule achukue hatua mara moja dhidi ya mtumishi husika.

5. Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Machi, 2023.

6. Nawatakia utekelezaji fanisi.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala**: Wathibiti Wakuu wa Ubora wa Shule Kanda na Wilaya

**TANZANIA BARA**